

**HOTUBA YA KATIBU MKUU KIONGOZI YA KUFUNGA MKUTANO
WA FARAGHA WA MAKATIBU WAKUU, MAKATIBU TAWALA WA
MIKOA NA NAIBU MAKATIBU WAKUU ULIOFANYIKA KATIKA
UKUMBI WA MIKUTANO WAJAKAYA KIKWETE, IKULU DAR ES
SALAAM, TAREHE 13 - 14 JULAI, 2022**

*Mha. Zena A. Said, Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu
Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar,*

Makatibu Wakuu,

Makatibu Tawala wa Mikoa,

Naibu Makatibu Wakuu,

Wakuu wa Taasisi,

Watoa Mada,

Wageni Waalikwa,

Mabibi na Mabwana.

Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania... Kazi
Iendele...!

Napenda nichukue fursa hii kuwashukuru wote kwa ushiriki wenu mzuri
katika siku hizi mbili za Mkutano ambao tunauhitimisha leo. Nimepata
faraja kwa namna mlivyoshiriki kwa ukamilifu katika majadiliano na
kutoa maoni na ushauri kwenye masuala mbalimbali yaliyojadiliwa.
Aidha, nawashukuru Watoa Mada wote kwa kuwasilisha mada kwa
weledi na umahiri. Mada hizo zimekuwa msingi wa kuwezesha kufanyika
kwa majadiliano yetu.

Kwa mara nyingine tena, nimshukuru Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kushiriki na kuwa nasi kwa siku zote za Mkutano pamoja na kwamba anayo majukumu mengi. Aidha, nawapongeza Kamati ya Maandalizi ya Mkutano huu kwa maandalizi mazuri ya Mkutano na huduma zilizotolewa wakati wote wa Mkutano huu.

Ndugu Washiriki,

Kama nilivyoeleza wakati wa ufunguzi, Mkutano huu ni wa kikanuni na umefanyika kwa lengo la kujadili na kubadilishana maarifa na uzoefu katika utekelezaji wa shughuli za Serikali Kuu; Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; pamoja na Mashirika ya Umma. Ni matumaini yangu kuwa, sote tunahitimisha Mkutano huu tukiwa na uelewa mpana zaidi kuhusu wajibu wetu kama Viongozi, na kwamba tutakwenda kutumia maarifa na uzoefu tuliopata katika kuimarisha utekelezaji wa majukumu yenu pamoja na kuimarisha utawala bora na uwajibikaji.

Ndugu Washiriki,

Mtakubaliana na mimi kuwa, Mkutano huu pia umetuwezesha kupata taarifa na uelewa zaidi kuhusu zoezi la Sensa ya Watu na Makazi linalotarajiwa kufanyika tarehe 23 Agosti, 2022. Kama nilivyoeleza wakati wa ufunguzi, Sensa hiyo itawezesha Serikali kubuni, kupanga na kutekeleza mipango ya uchumi na maendeleo kwa wananchi. Hivyo, ninyi mkiwa kama Watendaji Wakuu na wasimamizi wa shughuli za Serikali mna wajibu mkubwa wa kuhakikisha kuwa zoezi hilo linafanyika kwa ufanisi na mafanikio kama ilivyokusudiwa na Serikali.

Ndugu Washiriki;

Mmepata fursa ya kujadili Taarifa ya Tathmini kuhusu Mfumo wa Kubuni, Kupanga, Kuratibu na Kutekeleza Shughuli za Serikali na mmetoa maoni na ushauri wenu unaolenga kuboresha Mfumo huo. Maoni na ushauri uliolewa utafanyiwa uchambuzi wa kina ili kuwezesha Serikali kuendelea na hatua za kufanya maboresho ya mifumo yake ya Ubunifu, Upangaji Utekelezaji, Udhibiti, Ufuatiliaji na Tathmini.

Ndugu Washiriki;

Kupitia Mkutano huu, mmepata fursa pia ya kukumbushwa kuhusu wajibu wenu kama Maafisa Masuuli katika kusimamia matumizi ya rasilimali za umma. Hivyo, nasisitiza na kuwaelekeza kuwa, muendelele kuimarisha usimamizi wa rasilimali hizo na msisite kuchukua hatua za kisheria na kinidhamu dhidi ya wote watakaobainika kufanya ubadhirifu wa mali za umma.

Ndugu Washiriki;

Maazimo mbalimbali yaliyofikiwa na kukubaliana katika Mkutano huu hayana budi kutekelezwa na yawekewe mpango kazi wa kuyatekeleza. Kabla ya kuhitimisha, niwaeleze kuwa, kutokana na umuhimu wa mkutano huu, tutaendelea kupata fursa ya kuwa na mikutano ya namna hii kwa siku zijazo kwa lengo la kujadili masuala mengine muhimu yanayohusu utendaji wa Serikali na utoaji wa huduma kwa wananchi kwa ujumla wake.

Ndugu Washiriki;

Baada ya kueleza hayo, natamka kuwa Mkutano wetu umefungwa rasmi hadi wakati mwingine na niwatakie safari njema mnaporejea katika vituo vyenu vya kazi.

ASANTENI KWA KUNISIKILIZA!



Jiandae Kuhesabiwa Siku ya Jumanne tarehe 23 Agosti, 2022